**Journal of Kiswahili and Other African Languages**
Vol. 3 No. 2 (2025): ISSN (Online): 2958-4914
DOI: https://doi.org/10.58721/jkal.v3i2.1479
*Mtagusano wa Vipengele vya Utandawazi na Vipengele vya Falsafa ya Ubuntu katika Riwaya Teule za Kisasa za Kiswahili*

# Mtagusano wa Vipengele vya Utandawazi na Vipengele vya Falsafa ya Ubuntu katika Riwaya Teule za Kisasa za Kiswahili

**Bakita Malindi[1] & Anna Kyamba[2]**
[1]*Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Tanzania*
[2]*Chuo Kikuu Huria cha Tanzania*

***Uwasilishaji wa Makala***
Kupokelewa: 2025-06-14
Kurekebishwa: 2025-11-25
Kukubaliwa: 2025-11-30
Kuchapishwa: 2025-12-10

**Maneno Muhimu**
Mtagusano
Riwaya
Ubuntu
Utandawazi

***Jinsi ya Kurejelea Makala:***
Malindi, B., & Kyamba, A. (2025). Mtagusano wa Vipengele vya Utandawazi na Vipengele vya Falsafa ya Ubuntu katika Riwaya Teule za Kisasa za Kiswahili. *Journal of Kiswahili and Other African Languages*, *3*(2), 118-127.

Copyright © 2025
CC BY NC SA

**Ikisiri**
Riwaya za kisasa ni zile zilizoandikwa katika zama za utandawazi na huakisi maisha, changamoto, na mitazamo ya dunia ya sasa. Tofauti na riwaya zisizo za kisasa au za mwanzo zinazosawiri mfumo wa maisha unaowaunganisha Waafrika kuishi kwa umoja na kushirikiana katika shughuli mbalimbali za maendeleo (Mbaabu, 1985). Riwaya za mwanzo zilihusisha mambo mbalimbali kama vile kusifia uhuru, falsafa ya Ubuntu, na Azimio la Arusha. Kwa kuwa, falsafa ya Ubuntu ilikuwepo toka zamani, ilichunguzwa pia katika riwaya za mwanzo (Roman, 2019). Vilevile, kuna tafiti zimeonesha kuwa falsafa ya Ubuntu imepotea kipindi cha utandawazi (Masimo, 2023). Hivyo, shabaha ya makala hii ni kuonesha mtagusano wa vipengele vya utandawazi na vya falsafa ya Ubuntu katika riwaya za kisasa za Kiswahili. Inasemekana kuwa, uandishi wa riwaya za kisasa ulianza miaka 1990 hadi sasa, ingawa utafiti huu umehusisha riwaya za kisasa zilizoandikwa miaka 2000 hadi 2010. Hii ni kwa sababu, riwaya zilizoandikwa miaka hiyo ni za aina tofauti, kama vile riwaya za kihistoria, za kisasa, na za kisaikolojia (Mulokozi, 2017). Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Mwingilianomatini iliyoasisiwa na Julia Kristeva mwaka 1960. Data zilikusanywa na kuchambuliwa kwa kutumia mbinu ya usomaji makini wa matini zinazohusiana na utafiti ambazo ni riwaya za kisasa mbili za Kiswahili, nazo ni *Babu Alipofufuka* (2001) na *Makuadi wa Soko Huria* (2002). Riwaya hizo zimeteuliwa kwa sababu, zina sifa inayoendana na mada ya utafiti, na ni miongoni mwa riwaya za kisasa zilizoandikwa miaka 2000 mpaka 2010. Vilevile, data zilizopatikana zilifafanuliwa kwa kutumia mkabala wa kitaamuli. Aidha, matokeo ya utafiti huu yamedhihirisha kuwa vipengele vya utandawazi vimetagusana na vipengele vya falsafa ya Ubuntu katika riwaya za kisasa.

## Utangulizi

Fasihi ni sanaa inayotumia lugha kiubunifu ili kueleza tajiriba mbalimbali za maisha ya mwanajamii (Msokile, 1993). Senkoro (2007) anasema kuwa fasihi hubadilika kulingana na mabadiliko ya jamii. Mabadiliko hayo ndiyo husababisha kuibuka kwa namna mpya ya utunzi wa tanzu mbalimbali za fasihi kama vile riwaya. Sambamba na maelezo hayo, Khamis (2007) anadai kuwa riwaya ya kisasa ni mwondoko wa utanzu wa riwaya au hali ya kimajaribio ya riwaya kutoka sura iliyozoeleka kwenda sura mpya. Kwa ujumla, tunaweza kusema kuwa riwaya za kisasa ni aina za riwaya ambazo uandishi wake unachanganya mbinu za kijadi na mbinu za kisasa. Vilevile, usimulizi wake huwa si wa moja kwa moja (Mutua, 2022). Hali hii husababisha riwaya hizi kuwa ngumu kueleweka

kwa msomaji. Kimsingi, riwaya za kisasa zimepokea mabadiliko kimaudhui na kifani kutoka katika nyanja mbalimbali. Baadhi ya mabadiliko hayo yanatokana na utandawazi, na ndiyo hufanya riwaya za kisasa zionekane na upya kimaudhui na kifani. Naye, Selemani (2012) anaeleza kuwa riwaya za kisasa ni zile zenye maudhui mapya yanayosawiri hali ya ulimwengu wa sasa. Mifano ya hali hiyo ni masuala ya uvutaji bangi na madawa ya kulevya, ugaidi, ndoa za jinsia moja na biashara haramu. Kadhalika, Masimo (2023) anaeleza kuwa baadhi ya riwaya za mwanzo zilikuwa na sura ya kifasihi simulizi. Vilevile, zilichukua mambo mengi kutoka katika jamii ya Kiafrika. Anaongezea kuwa tunaposema riwaya za mwanzo tunamaanisha riwaya zilizoandikwa miaka ya 1980 kurudi nyuma. Aidha, riwaya hizo zinaonekana kusawiri maisha ya jamii katika nyanja za kiutamaduni, kiuchumi, na kisiasa. Jambo ambalo bado lipo katika riwaya za kisasa, licha ya riwaya hizo kuwa na sifa ya kuandika masuala ya kijamii, kisiasa na kiuchumi kwa kujikita katika utamaduni wenye sura ya utandawazi. Hata hivyo, riwaya za kisasa zimedumu kwa muda mrefu takribani miaka 35 hivi tangu kuanza hadi sasa, ingawa katika utafiti huu tumejikita na zile zilizoandikwa kuanzia miaka ya 2000 hadi 2010. Hivyo, makala hii imechunguza mtagusano uliopo kati ya vipengele vya utandawazi na vipengele vya falsafa ya Ubuntu ambavyo vinajitokeza katika riwaya teule za kisasa za Kiswahili. Katika maelezo yanayofuata tumefafanua istilahi muhimu katika utafiti huu ambazo ni mtagusano, utandawazi, na falsafa ya Ubuntu.

Kwa mujibu wa BAKITA (2017), mtagusano ni hali ya vitu viwili kuingiliana. Hivyo, katika makala hii tunazungumzia mwingiliano wa vipengele vya utandawazi na vipengele vya falsafa ya Ubuntu uliobainika katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* (2001) na *Makuadi wa Soko Huria* (2002). Kwa kuwa utafiti huu umehusisha utandawazi na falsafa ya Ubuntu, ni vema kuelezea kuhusiana na istilahi hizi. Oruka (2012) anaeleza falsafa ya Ubuntu kuwa ni fikra au mitazamo wanayoishughulikia Waafrika wenyewe au watu wengine ambao wanakubali mila na desturi za Kiafrika. Naye Samweli (2015), anasema kuwa falsafa ya Ubuntu imetokana na mila na utamaduni wa Kiafrika, ambao umejengwa juu ya maslahi ya jamii zaidi ya maslahi ya mtu binafsi. Kwa ujumla, falsafa ya Ubuntu ni dhana au mawazo ya Waafrika wenyewe juu ya mambo mbalimbali wanayoyafanya. Mfano wa mambo hayo ni imani juu ya maisha, mila, desturi, jinsi ya kushirikiana katika jamii, na kutafuta suluhisho juu ya matatizo yanayowakabili. Kwa upande mwingine, utandawazi ni hali ya kimahusiano ya kijamii inayoruhusu kuondolewa kwa vikwazo vya kijiografia katika masuala ya kiuchumi, kisiasa, na katika miundo ya kijamii na kiutamaduni, ambapo watu huwa wanaelewa, na huwa sehemu katika mabadiliko hayo (Waters, 2001). Naye Thomas (2005) anaeleza kuwa utandawazi ni mchakato wa kuunganisha uchumi, siasa, jamii, na uhusiano wa tamaduni baina ya nchi mbalimbali. Kwa ujumla, katika makala hii tunachukulia utandawazi kuwa ni mwingiliano uliopo kati ya nchi za Kiafrika na mataifa mengine katika mambo ya kiuchumi, kiutamaduni, kielimu, na kijamii, unaoifanya dunia kuwa kama kijiji.

Sambamba na maelezo hayo, katika zama hizi za utandawazi wamejitokeza watafiti wengi waliochunguza riwaya kwa kuegemea zaidi katika suala la utandawazi. Miongoni mwa watafiti hao ni: Mulokozi (2006), Kalegeya (2012), Kevogo (2017), Mwangi (2022), na Masimo (2023). Mambo yanayoelezwa na watafiti hawa ni: jinsi utandawazi ulivyoathiri falsafa ya Ubuntu wa jamii za Kiafrika na kusababisha kuporomoka kwa maadili; na hali ya usasa kuwa chanzo cha uharibifu wa mifumo ya familia za Kiafrika. Hata hivyo, utandawazi ulipoingia barani Afrika umetagusana na vipengele mbalimbali vya falsafa ya Ubuntu, ambavyo vilikuwepo tangu zamani katika jamii ya Kiafrika. Vipengele vya utandawazi vilivyobainika katika utafiti huu ni: biashara ya magendo, soko huria, umilikishwaji ardhi, utamaduni wa kigeni, uhuru wa vyombo vya habari, na uanzishwaji wa miradi mbalimbali. Vilevile, vipengele vya falsafa ya Ubuntu vilivyobainika ni: haki, heshima,

ukarimu, huruma, adabu njema, umoja na ushirikiano. Kwa ujumla, katika utafiti huu tumeonesha jinsi vipengele hivyo vilivyotagusana. Sehemu ifuatayo inahusu nadharia iliyouongoza utafiti huu.

## Nadharia ya Utafiti

Utafitii huu, uliongozwa na Nadharia ya Mwingilianomatini iliyoasisiwa na Mwanasemiotiki wa Kifaransa, Julia Kristeva mnamo mwaka 1960. Baadaye nadharia hii iliendelezwa na Fairclough mwaka 1992. Kristeva alibuni dhana ya Mwingilianomatini kwa kuhusisha dhana ya de Saussure ya kiisimu ya Semiotiki, na dhana ya Usemezano ya Mikhail Bakhtin (1895 – 1975). Bakhtin katika nadharia hiyo ya usemezano anaamini kuwa, kazi ya fasihi ina sauti mbalimbali zinazoingiliana na kupiga mwangwi katika kazi nyingine zilizotangulia, zilizopo, na zitakazokuja baadaye. Hii ina maana kuwa athari ya kazi moja huweza kuonekana katika kazi nyingine zilizotangulia, zilizopo, na hata zijazo. Kristeva aliyaendeleza mawazo ya Bakhtin na kuibua Nadharia ya Mwingilianomatini mnamo mwaka 1960. Dhana kuu katika nadharia hii ni kuwa, hakuna matini ya kifasihi inayoweza kujitegemea bila kuhusiana na matini nyingine. Kwa mantiki hiyo, matini zote huhusiana kwa njia moja ama nyingine, na vilevile, matini zenyewe hutegemeana ili kuzalisha maana. Hivyo, msanii hutunga matini yake kutokana na matini za awali (Kristeva, 1978).

Aidha, Nadharia ya Mwingilianomatini ina mihimili mikuu kadhaa ambayo inaisimamia. Kwa mujibu wa Ngesa, Matundura, na Kobia (2016), baadhi ya mihimili mikuu ya nadharia hii ni pamoja na:

1. Kila matini ni mwingiliano wa matini mbili au zaidi;
2. Kazi za fasihi hupatikana kwa kuhusianisha na matini zingine za kifasihi au zisizo za kifasihi.

Hivyo basi, utafiti wa makala hii uliongozwa na mihimili miwili ya Nadharia ya Mwingilianomatini. Mihimili hiyo iliwaongoza watafiti kuchambua maudhui katika riwaya za kisasa ili kubainisha vipengele vya utandawazi na vipengele vya falsafa ya Ubuntu vilivyotagusana katika riwaya teule za kisasa za Kiswahili.

## Methodolojia ya Utafiti

Katika utafiti huu, wango ni riwaya za kisasa za Kiswahili zote zilizoandikwa kuanzia miaka 2000 hadi 2010. Vilevile, sampuli iliyotumika ni riwaya za kisasa mbili za Kiswahili zilizoandikwa kuanzia miaka 2000 hadi 2010. Riwaya hizo ni *Babu Alipofufuka* (2001) na *Makuadi wa Soko Huria* (2002). Riwaya hizo zimeteuliwa kwa sababu ni miongoni mwa riwaya za kisasa za Kiswahili zilizoandikwa kuanzia mwaka 2000 hadi 2010. Hata hivyo, uteuzi wake ulitumia mbinu ya usampulishaji lengwa. Mtafiti ametumia mbinu ya usampulishaji lengwa kuchagua riwaya zilizokuwa na sifa kulingana na mada ya utafiti huu. Vilevile, alibaini kuwa riwaya hizo zitamwezesha kukidhi malengo ya utafiti. Data za utafiti zilikusanywa na kuchambuliwa kwa kutumia mbinu ya usomaji makini wa matini, ambapo mtafiti alisoma kwa umakini riwaya hizo, kisha akachambua data zinazohusiana na utafiti wake. Aidha, data zilizopatikana zilifafanuliwa kwa kutumia mkabala wa kitaamuli. Mkabala huu hutumia zaidi ufafanuzi wa maelezo katika kuhusisha taarifa mbalimbali za kitafiti.

## Matokeo ya Utafiti

Sehemu hii inabainisha vipengele vya utandawazi na falsafa ya Ubuntu na jinsi vilivyotagusana kwa kutumia riwaya ya *Babu Alipofufuka* (2001) na *Makuadi wa Soko Huria* (2002). Vipengele vilivyobainishwa katika makala hii ni; (1) Haki, soko huria, na umilikishwaji wa ardhi, (2) Heshima, na utamaduni wa kigeni, (3) Umoja, Ushirikiano, Ubinafsishaji, na Uwekezaji, na (4) Huruma, utamaduni wa kigeni, na biashara ya magendo. Kupitia vipengele hivyo tulivyovibainisha,

tumeonesha dhahiri jinsi mtagusano wa vipengele vya utandawazi, na vya falsafa ya Ubuntu unavyojitokeza katika riwaya teule za kisasa za Kiswahili. Mtagusano huo unathibitisha dai la msingi la Nadharia ya Mwingilianomatini lililowekewa msingi na Julia Kristeva kuwa hakuna matini inayoweza kuangaliwa kivyake au kipekee, pasipo kuhusishwa na matini nyingine. Hivyo, misingi ya Nadharia ya Mwingilianomatini imetuongoza katika uchambuzi wa vipengele vilivyobainishwa hapo juu.

***Haki, Soko Huria na Umilikishwaji wa Ardhi***

Haki ni jambo ambalo mtu anastahiki au kitu anachostahiki kuwa nacho (TUKI, 2019). Haki ndio msingi wa maendeleo ya watu. Haki hutokea pale ambapo mtu anafanya jambo analoamini kuwa hamwonei mtu bali ni stahiki yake kufanya hivyo. Aidha, soko huria ni kipengele cha utandawazi, kinachoonesha uhuru wa biashara katika enzi hizi za utandawazi. Halikadhalika, umilikishwaji ardhi ni kipengele cha utandawazi kinachoonesha tendo la kujitwalia ardhi ya watu fulani, na kuiweka katika umiliki wa mtu au watu binafsi (Chachage, 2002). Haki ni kipengele cha falsafa ya Ubuntu ambacho kimetagusana na soko huria kikiwa ni kipengele kimojawapo cha utandawazi. Mdhihiriko huu wa mtagusano, tumeuonesha hapa chini kama ifuatavyo:

Katika riwaya ya *Babu Alipofufuka*, mwandishi amezungumzia suala la haki pale alipomtumia mhusika Babu Mzuka. Mhusika huyu aliongea na K na wageni kutoka nje kuwa haki lazima itendeke kwa kila mtu, na si kwamba haki iambatane na pesa, bali ifuatwe katika misingi ya usawa. Katika kuelezea suala la haki, mwandishi ameonesha jinsi haki ilivyotagusana na biashara huria. Hii imedhihirika wakati Babu Mzuka alipowasisitiza K na wageni kutoka nje ya nchi, kuhusiana na haki na misingi ya usawa, katika kikao cha kujadili mradi wa FKK. Mwandishi amezungumzia mtagusano wa haki na soko huria pale Babu Mzuka anaposema:

> Mkubali biashara kwa upana wake na utamaduni wa msingi wa kufungua milango. Msingi wa haki. Na haki si haki za kawaida tu, bali pia haki za maraha, haki za watu kufanya wapendavyo… haki ya kuvaa wapendavyo … haki ya mwanamke kuzaa na mume maiti, haki ya kuzalishwa watu kwa sindano… haki na haki na haki … (uk. 44).

Nukuu hii inaonesha jinsi haki ilivyotagusana na biashara huria. Mtagusano huo unathibitisha uwepo wa mwingiliano wa vipengele hivyo. Kama asemavyo Kristeva (1978) kuwa kila matini ni mwingiliano wa matini mbili au zaidi. Hii imedhihirika pale Babu Mzuka alipowasisitiza akina K na wageni kutoka nje ya nchi walipokuwa wanajadili kuhusiana na soko huria katika mradi wa FKK. Wakati wanajadili Babu Mzuka alitokea na kusisitiza kuhusu haki, kwamba haki itendeke katika misingi ya usawa na kusiwe na upendeleo. Naye, Mohamed (2001) anasisitiza kwamba suala la haki lisiambatane na pesa, cheo na hata kujuana, bali haki ifuate misingi ya usawa.

Halikadhalika, suala la haki limesawiriwa katika riwaya ya *Makuadi wa Soko Huria*, kwa kuwatumia wanakijiji wanawake wa kijiji cha Ruhimba akiwamo Binti Wenga. Mhusika huyu na wenzake walitaka kudhulumiwa haki yao ya ardhi na uongozi wa wilaya, pamoja na matajiri wageni kutoka mjini. Binti Wenga na wanawake wenzake wakaungana na kukubaliana kwamba, mtu mmoja aende kupeleka kero yao bungeni ili wasidhulumiwe haki yao ya kumiliki ardhi. Kipengele cha haki kimetagusana na kipengele cha umilikishwaji wa ardhi ambacho ni kimojawapo ya vipengele vya utandawazi. Viongozi na wageni kutoka mjini walitaka wajimilikishe ardhi ya akina Binti Wenga kwa dhuluma. Haya yanadhihirika mwandishi anaposema:

> Lakini kwa sababu huu ni msimu wa kulima, tukakubaliana kwamba mtu mmoja aupeleke ujumbe wa kero yetu bungeni. Mimi (Binti Wenga) nilijitolea kuuwasilisha huo ujumbe (uk. 42).

> … tulimhitaji mbunge ili aje atutetee dhidi ya uongozi wa wilaya ulionyang'anya mashamba mengi ya wanawake na kununua kwa malipo ya haki yale yenye nyumba zenye wanaume. Walidai kwamba ardhi ni mali ya taifa, na sasa serikali iliyahitaji mashamba hayo kwa ajili ya mradi wa uchumi … (uk. 45).

Nukuu hii inaonesha mtagusano wa haki na umilikishwaji ardhi. Kwa kuongozwa na Nadharia ya Mwingilianomatini tunaona jinsi wanawake wa kijiji cha Ruhimba walivyotambua haki yao ya umiliki wa ardhi. Hii ni kutokana na kwamba, baadhi ya viongozi, matajiri na wageni kutoka mjini walitaka kudhulumu haki ya wanakijiji, kwa kujimilikisha ardhi yao. Jambo hili walilifanya kwa kisingizio kuwa wanawake hawana haki ya kumiliki ardhi. Mwandishi anatoa funzo kwa jamii kuwa haki itendeke kwa watu wote, na tusitumie madaraka, nyadhifa, na utajiri tulionao kudhulumu haki ya wengine.

***Heshima, utamaduni wa kigeni na vyombo vya habari***

Heshima ni kipengele cha falsafa ya Ubuntu ambacho kinahusu suala la nidhamu kwa watu wa rika zote. Heshima ni mwenendo mwema, adabu, thamani anayopewa mtu machoni mwa jamii (BAKITA, 2017). Aidha, Kalegeya (2012) anasema utamaduni ni jumla ya mambo yote yanayokamilisha maisha ya mwanadamu ya siku hata siku. Utamaduni unajumuisha mambo kama vile lugha, mavazi, chakula, imani, kucheza, na kadhalika. Katika kipindi cha utandawazi baadhi ya Waafrika wamekuwa wakipuuza utamaduni wao na kufuata ule wa kigeni. Jambo ambalo limeleta mabadiliko makubwa katika utamaduni wa asili na kuibuka kwa utamaduni wa kigeni katika jamii mbalimbali za Kiafrika (Masimo, 2023). Vilevile, kipengele cha heshima kimetagusana na utamaduni wa kigeni ambacho ni kipengele kimojawapo cha utandawazi. Mtagusano huo umedadavuliwa vizuri hapa chini, ambapo:

Kwa kutumia riwaya ya *Babu Alipofufuka*, mwandishi amewatumia wahusika wasichana wakaribishaji kuonesha jinsi heshima inavyojitokeza baina yao na Bwana K. Wasichana wakaribishaji walitoa heshima kwa K na watukufu wengine walipokuwa wakiingia katika jengo la *New Casino*. Wasichana hao walikuwa na nywele ndefu za dhahabu zilizomiminika upande mmoja pindi walipogeuka na kuzirudisha upande mwingine. Hapa tunaona jinsi kipengele cha heshima kilivyotagusana na utamaduni wa kigeni. Wasichana hao walikuwa wamevaa mavazi mafupi yanayoonesha maungo ya miili yao, na nywele za dhahabu zilizomiminika pindi walipogeuka. Haya yanadhihirika mwandishi anaposema:

> Vitovu vilikuwa vimechorwa kwa mzunguko, nembo ya tattoo ya jua lenye kutoa miale. Kiini cha kitovu kilionekana kuchekelea. Walipoinama kutoa heshima, nywele zao za dhahabu na haramu ya singa zilimiminika upande mmoja, wakajitikisa kuzipungia upande mwengine kama wafanyavyo *wenyesinga zao* (uk. 32).

Kupitia nukuu hii, mwandishi ameonesha jinsi heshima ilivyotagusana na utamaduni wa kigeni. Kwa kuongozwa na Nadharia ya Mwingilianomatini katika mhimili mmojawapo ni dhahiri kuwa hakuna matini inayoweza kuangaliwa kipekee bila kuhusisha na matini nyingine (Kristeva, 1978). Hivyo, kipengele cha heshima kinamwingiliano na utamaduni wa kigeni katika riwaya teule. Kwa ujumla, tunaweza kusema kuwa katika enzi hizi za utandawazi, baadhi ya vipengele vya falsafa ya Ubuntu vinajitokeza kwa kuingiliana na vipengele vya utandawazi.

Vilevile, katika riwaya ya *Makuadi wa Soko Huria*, heshima na vyombo vya habari ni vipengele vilivyodhihirisha mtagusano wa falsafa ya Ubuntu na utandawazi. Mwandishi anawatumia wataalamu wa vyombo vya habari kusisitiza suala la heshima, haki, unyoofu, na uadilifu, ili kuwe na nuru ya matamanio ya harakati za maisha. Mwandishi amemtumia mhusika Fidelis, ambaye ni

mwandishi wa habari mwenye hamu ya kuueleza umma kuhusiana na suala la heshima na haki. Fidelis anaamini kwa kutumia vyombo vya habari, watu huweza kupata ujumbe na kuuishi, ijapokuwa uhuru wa vyombo vya habari ulibanwa. Haya yanajitokeza uk wa 13, mwandishi anaposema:

> Nilitarajia kuanzisha gazeti ambalo lingetoa habari na makala ambazo zingekuwa kioo cha maisha ya Watanzania, ambalo lingeakisi udhaifu wao na kuwafanya wajikosoe, liwaumbue maaluni, wale wenye uwili wa popo wa kujifanya ndege kumbe ni wanyama, mazandiki na waovu … Lingerudisha tena nuru ya matamanio ya uadilifu, haki na heshima (uk. 13).

Kupitia nukuu hiyo, tunaona jinsi vipengele vya heshima na vyombo vya habari vilivyotagusana. Hata hivyo, kwa mujibu wa Nadharia ya Mwingilianomatini katika mhimili mmojawapo, ni dhahiri kuwa kipengele cha heshima na vyombo vya habari vimetagusana. Jambo hili limedhihirika kwa kuwa kazi za kifasihi hupatikana kwa kuhusianisha na matini zingine za kifasihi au zisizo za kifasihi. Hapa tunachukulia kwamba vipengele hivyo ni kazi za kifasihi, ambapo vinahusiana katika ujenzi wa matini. Kwa kuhitimisha, mwandishi alimtumia Fidelis kuonesha jinsi vyombo vya habari vilivyohusianishwa na heshima kwa pamoja, kisha kujenga dhima ya kuuelimisha umma uliokwenda kinyume, ili kujirudi katika misingi ya haki na heshima.

***Umoja, Ushirikiano, Ubinafsishaji, na Uwekezaji***

Umoja na ushirikiano ni kipengele kingine cha falsafa ya Ubuntu kilichotagusana na ubinafsishaji na uwekezaji ambavyo ni vipengele vya utandawazi. Roman (2019) anasema kuwa umoja na ushirikiano ni kitendo cha mtu kukubaliana na watu wengine katika kufanya jambo kwa pamoja. Anaendelea kusema umoja huwaunganisha watu na kuwaweka pamoja katika shughuli mbalimbali wazifanyazo. Kwa upande mwingine, TUKI (2019) inasema uwekezaji ni kitendo cha kuweka kitegauchumi kwa lengo la kuzalisha mali. Vilevile, Selemani (2012) anasema ubinafsishaji ni hali ya kufanya mali ya umma kuwa ya binafsi. Kwa ujumla, ubinafsishaji ni kitendo cha kujimilikisha mali kwa faida yako bila kujali wengine. Kwa kutumia riwaya teule za kisasa, tumeonesha jinsi vipengele hivi vinavyotagusana.

Katika riwaya ya *Babu Alipofufuka*, kipengele cha umoja na ushirikiano kimetagusana na kipengele cha ubinafsishaji. Mwandishi amefanikiwa kuzungumzia haya pale alipoonesha kuwa umoja na ushirikiano ni kipengele muhimu sana cha kuwaunganisha watu pamoja na kujenga nguvu moja kwenye umoja wao. Aidha, umoja na ushirikiano huwafanya watu waishi pamoja bila kuparaganyika. Hali hii imedhihirika pale K na wageni kutoka nchi za nje waliposhirikiana katika kuhimiza umoja wa kundi lao. Lengo la kundi hilo ni kujibinafsisha ardhi kubwa ili waanzishe klabu ya FKK kwa maslahi yao binafsi. Mwandishi anasema:

> Tokea mwanzo ulikuwepo mwanya mkubwa kwa hakika, lakini wote walifumba vijaluba vyao, kwa madhumuni ya kuhami maslahi yao na kujenga nguvu kwenye umoja wao. Vyenginevyo wangeparaganyika (uk. 45).
>
> "Kwani ndo mradi umeshakubalika?" Aliuliza Bwana Tajuri. Ni kitu kipya FKK, na kitu kipya kina uzuri wake, hasa kibiashara … Isitoshe lazima mtambue kwamba kufungua milango kuna kanuni zake (uk. 44)

Dondoo hili linaonesha jinsi vipengele vya umoja na ushirikiano, ubinafsishaji, na uwekezaji vilivyotagusana. Kwa kuongozwa na Nadharia ya Mwingilianomatini tunaona jinsi vipengele vya umoja na ushirikiano, ubinafsishaji, na uwekezaji vinavyoingiliana katika riwaya teule za kisasa. Mwingiliano huo hudhihirika kwa kuwatumia wahusika K, Von Heim, Tajuri na wageni kutoka

nchi za nje. Wahusika hawa walishirikiana kwa pamoja, kujadili uanzishwaji wa mradi kwa ajili ya kujiongezea kipato chao binafsi.

Halikadhalika, riwaya ya *Makuadi wa Soko Huria*, inadhihirisha mtagusano kati ya umoja, ushirikiano na uwekezaji. Mtagusano huo hudhihirika kwa kuwatumia wahusika mbalimbali kama vile Japhet Lupocho, Amina na wavuvi. Japhet Lupocho alishirikiana vizuri na wavuvi aliowapa kazi ya kumkusanyia samaki kwa ajili ya kiwanda cha East African Investment. Lupocho aliwalipa vizuri na kwa wakati wavuvi hao. Vilevile, Lupocho alishirikiana vizuri na Amina katika biashara ya samaki. Mwandishi amedhihirisha haya kwa kusema:

> Na ni kwa njia hiyo aliweza kutamba kwamba alikuwa amepanga nyumba ya East African Investment akiwa Rufiji, ili kuwaonyesha watu kuwa, hali yake ya kifedha ilikuwa nzuri, kama alivyowalipa wavuvi vizuri (uk. 166)
>
> Watu walichukulia kwamba ni mahusiano ya tajiri na mteja, na hata wale waliosikia fununu za huo uhusiano, mara kwa mara, walichukulia kwamba, ni habari za kuvumisha tu (uk. 167)

Dondoo hilo linaonesha jinsi mtagusano wa ushirikiano na uwekezaji ulivyojitokeza. Uchambuzi huu umeongozwa na Nadharia ya Mwingilianomatini katika mhimili unaosisitiza kuwa kazi mpya hujengwa kwa kuhusianisha kazi mbili au zaidi. Hivyo, ni dhahiri kuwa Japhet Lupocho alionesha ushirikiano mzuri kwa wafanyakazi wake pale alipowalipa mshahara kwa wakati. Aidha, wafanyakazi hao walikusanya samaki kwa uangalifu, kwa ajili ya kupeleka katika kiwanda cha kusindika samaki. Vilevile Lupocho alionesha ushirikiano kati yake na Amina aliyekuwa mfanyabiashara wa samaki. Amina alifanya biashara ya samaki kwa uaminifu, ambapo Lupocho alinunua samaki hao na kupeleka kiwandani.

***Huruma, Utamaduni wa Kigeni na Biashara ya Magendo***

Huruma ni kipengele cha falsafa ya Ubuntu kilichotagusana na utamaduni wa kigeni, biashara ya magendo na uanzishwaji wa mradi wa kamba. Huruma ni hali ya kuchukulia changamoto ya mtu mwingine na kuifanya kama yako, kwa maneno mengine, huruma ni moyo wa kutenda mema; moyo wa imani; hisia ya kupenda kusaidia watu wengine; rehema na upole (TUKI, 2019). Biashara ya magendo ni kitendo cha ununuzi na uuzaji wa bidhaa kwa njia isiyo halali (BAKITA, 2017). Katika utafiti huu biashara hiyo imefanyika kwa siri kwa matajiri wakubwa ili kukwepa ulipaji wa kodi. Maelezo yafuatayo yanaonesha jinsi huruma ilivyotagusana na vipengele vya utandawazi kwa kutumia riwaya teule za Kiswahili:

Katika riwaya ya *Babu Alipofufuka*, huruma na utamaduni wa kigeni ni vipengele vilivyodhihirika kutagusana. Huruma imejitokeza pale ambapo Bwana K alikutana na jibwa lake maarufu kama Doggy, baada ya kupotezana kwa muda mrefu. Bwana K alikuwa na huruma kwa Doggy na kuanza kufikiria aliishije, na chakula alipewa na nani. Baadaye K alikumbuka kuwa Biye aliyewasaidia kazi ni mtu mwenye huruma, hivyo siyo rahisi kumnyima Doggy chakula. Hivyo, ni lazima Doggy alipata chakula kama kawaida pamoja na mahitaji mengine. Kwa upande mwingine, K alionesha kuiga utamaduni wa kigeni pale alipomjali Doggy kuliko binadamu wenzake. Alithamini kumpa Doggy chakula na mahitaji mengine wakati binadamu wengine wakilala na njaa na kukosa mahitaji mengine muhimu. Vilevile, baada ya kupotezana na Doggy kwa muda mrefu, walipokutana, K alimkumbatia Doggy. Hapa utamaduni wa kigeni umedhihirika. Mwandishi anasema:

> Alizungusha ufunguo kitasani na kufungua mlango hatimaye; na mtu na jibwa lake wakakutana njiani. Wakavaana na kukumbatiana, kubusiana na kurambana. K machozi

> yalishaanza kumlengalenga, alimtaka sana samahani mbwa wake. Basi, basi Doggy wangu … basi! Masikini we … masikini … Hatujakutana mwaka mzima doggy wangu (uk.149).

Kupitia nukuu hii tunaona jinsi kipengele cha huruma kilivyotagusana na utamaduni wa kigeni. Kwa kuongozwa na Nadharia ya Mwingilianomatini tunaona jinsi K alivyokuwa na huruma kwa Doggy wake. K alifikiria kuwa Doggy aliishije wakati alipokuwa safarini, na mahitaji mengine aliyapataje. Aidha, K alionesha utamaduni wa kigeni baada ya kukutana na Doggy alikumbatiana na kunyonyana ndimi, jambo ambalo ni tofauti kabisa na utamaduni wa Kiafrika. Kwa ujumla, vipengele vya huruma na utamaduni wa kigeni vimehusianishwa katika kujenga matini mpya.

Vilevile, katika riwaya ya *Makuadi wa Soko Huria,* kipengele cha huruma kimetagusana na uanzishwaji wa miradi. Huruma imejitokeza pale ambapo Binti Miraji na mumewe walidhani kuwa Amina alikuwa anaelewa kuhusu uanzishwaji wa mradi huko Rufiji. Hii ni kutokana na kuwa, Lupocho aliyekuwa mpenzi wa Amina, alitoa mapendekezo ya kutetea kuhusu uanzishwaji wa mradi. Kumbe Amina hakujua chochote, na baada ya kuulizwa yaliyojiri mkutanoni alishangaa. Binti Miraji alimwangalia Amina kwa huruma, ingawa alisema sijui kama wengine hasa Shomari ataamini. Mwandishi anasema:

> Binti Miraji alimwangalia Amina pima machoni akitafuta dalili zozote za kumhaini katika yale aliyoyasema, kisha akasema. Sijui kwa nini nadhani unasema ukweli. Nakuonea huruma, ikiwa wengine hawatakuamini, na hasa kaka Shomari, kama ameyasikia haya basi uko matatani (uk. 172).

Dondoo hilo linadhihirisha mtagusano uliojitokeza kati ya huruma na uanzishwaji wa mradi. Binti Miraji na mumewe walimwonea huruma Amina aliyetelekezwa na mpenzi wake Lupocho. Lupocho alienda kuhudhuria kikao ili atetee uanzishwaji wa mradi wa kamba huko Rufiji. Kitendo hiki kiliwachukiza wakazi wa Rufiji kwa kuwa walidhani Lupocho ni mwenzao, kumbe aliwasaliti na kuwa upande wa wawekezaji wa mradi. Hata hivyo, kwa mujibu wa mhimili unaosema kuwa kila matini ni mwingiliano wa matini mbili au zaidi, ni dhahiri kuwa vipengele hivyo vimeingiliana katika kujenga matini.

Halikadhalika, kipengele cha huruma ambacho ni cha falsafa ya Ubuntu, kimetagusana na kipengele cha biashara ya magendo kikiwa ni miongoni mwa vipengele vya utandawazi. Hapa mwandishi anaonesha jinsi Chaurembo alivyomwonea huruma Sadiki baada ya kumwomba msamaha pale alipommwagia bia. Sadiki alibuni mbinu ya kumwaga bia ya Chaurembo kwa makusudi. Hii ni kutokana na kwamba Sadiki alimwekea dawa za kulevya Chaurembo ili aweze kumchukulia pesa na nyaraka za biashara ya magendo. Baada ya matendo hayo, Chaurembo alijilaumu kufanya kazi na mtoto mdogo kiasi hicho. Mwandishi anasema:

> Sadiki naye aliamua kuwa mnyenyekevu kwa kiasi fulani, “Mzee samahani. Kweli nilidhani nimeingiliwa na mdudu. Naomba unisamehe.” Chaurembo alimwangalia kwa huruma kidogo, na kujilaani kwa kiasi fulani kwa kujikuta akifanya biashara na mtoto mdogo kama yule. Akajiona mharibifu wa kupita kiasi, hadi kudiriki kufanya hizi shughuli na watoto wadogo (uk. 184-185).

Dondoo hilo linaonesha mtagusano uliojitokeza kati ya huruma na biashara ya magendo. Kwa kuongozwa na Nadharia ya Mwingilianomatini tumeona jinsi Chaurembo aliyejihusisha na biashara ya magendo, alivyomwonea huruma Sadiki. Hii ni kutokana na kwamba Sadiki alifanya mbinu ya kumwekea madawa ya kulevya katika bia yake. Sadiki aliamua kumwaga bia hiyo kwa makusudi

ili asigundulike kwa kitendo hicho. Hapo ndipo Sadiki alipomwomba Chaurembo msamaha, na Chaurembo alimwonea huruma na kumsamehe.

**Mjadala wa matokeo ya Utafiti**

Matokeo ya utafiti yameonesha kwamba kuna mtagusano wa vipengele vya utandawazi na falsafa ya Ubuntu katika riwaya teule za Kiswahili. Matokeo haya yanamaanisha kwamba katika enzi hizi za utandawazi falsafa ya Ubuntu nayo inajitokeza kwa kuendana na nyakati za sasa. Matokeo haya yanatofautiana na utafiti uliofanywa na Masimo (2023) anayesema kwamba utandawazi umeathiri falsafa ya Ubuntu wa jamii za Kiafrika na kusababisha kupotea kwa falsafa ya Ubuntu. Vilevile matokeo haya yanakubaliana na Nadharia ya Mwingilianomatini iliyotuongoza katika kutafiti mtagusano wa vipengele vya utandawazi na vipengele vya falsafa ya Ubuntu katika riwaya teule za kisasa za Kiswahili. Kimsingi, nadharia hii inapinga wazo la matini kujitenga, kujitegemea, na kujitawala, bali inasisitiza kwamba matini haiwezi kusimama yenyewe bila kuhusisha nyingine (Alfaro, 1996 & Allen, 2000). Kwa mantiki hiyo, utafiti huu ulihusisha mtagusano wa vipengele vya utandawazi na vya falsafa ya Ubuntu katika riwaya teule. Hivyo ni dhahiri kuwa vipengele hivyo vimekamilishana au kuingiliana ili kujenga kazi mpya, kama asemavyo Allen (2000) kuwa kazi za fasihi hupatikana kwa kuhusianisha na matini zingine za kifasihi au zisizo za kifasihi.

**Hitimisho**

Kimsingi, shabaha ya makala hii ilikuwa ni kutafiti mtagusano wa utandawazi na falsafa ya Ubuntu katika riwaya teule za kisasa za Kiswahili. Matokeo katika utafiti huu, yameonesha vipengele vya utandawazi na vipengele vya falsafa ya Ubuntu jinsi vilivyotagusana. Vipengele hivyo ni:

1. Haki, soko huria, na umilikishwaji wa ardhi;
2. Heshima na utamaduni wa kigeni;
3. Umoja, Ushirikiano, Ubinafsishaji, na Uwekezaji; na
4. Huruma, utamaduni wa kigeni, na biashara ya magendo.

Aidha, matokeo yamedhihirisha kuwa falsafa ya Ubuntu ipo kwa sura mpya ya kutagusana na vipengele vya utandawazi katika enzi hizi za utandawazi.

**Marejeleo**

Alfaro, M. J. M. (1996). Intertextuality: Origins and Development of the Concept. *Atlantis, Juz*. 18(1), 268-285.
Allen, G. (2000). *Intertextuality.* Routledge.
BAKITA. (2017). *Kamusi Kuu ya Kiswahili*. Longhorn Publishers (T) Ltd.
Chachage, C. L. (2002). *Makuadi wa Soko Huria*. Dar es Salaam University Press.
Kalegeya, T. (2012). Riwaya ya Kiswahili na Utandawazi: Uchunguzi wa *Makuadi wa Soko Huria* na *Almasi za Bandia* (Tasinifu ya Umahiri). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
Kevogo, A. U. (2017). Taswira ya Utandawazi katika Riwaya Mpya ya Kiswahili: Mfano wa Riwaya ya *Dunia Yao*. *Kioo cha Lugha*, 15, 41-56.
Khamis, S. A. M. (2007). Vionjo vya Riwaya ya Kiswahili. *Kioo cha Lugha*, 5, 18-27.
Kristeva, J. (1978). *Desire in Language: A Semiotic Approach to Literature and Art.* Columbia University Press.
Masimo, D. B. (2023). Mkengeuko wa Utamaduni wa Waswahili katika Riwaya ya Kiswahili zama za Utandawazi (Tasnifu ya Umahiri). Chuo Kikuu cha Dodoma.
Mbaabu, I. (1985). *Utamaduni wa Waswahili*. Kenya Publishing & Marketing
Mohamed, S. A. (2001). *Babu Alipofufuka*. Jomo Kenyatta Foundation.
Msokile, M. (1993). *Miongozo ya Lugha na Fasihi: Uchambuzi na Uhakiki wa Riwaya*. TUKI.

Mulokozi, M. (2006). Fasihi ya Kiswahili na Utandawazi. *Makala ya Kongamano la kimataifa la Jubilei ya TUKI 2005: Kuadhimisha Miaka 75 ya Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (1930 – 2005).*
Mulokozi, M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Moccony Printing Press.
Mutua, J. (2022). Riwaya za Kimajaribio: Burudani au Kikwazo kwa Msomaji? Mfano wa Riwaya Teule za K. W. Wamitila. *International Journal of Advanced Research*, 10(5), 468-478.
Mwangi, J. (2022). Uhakiki wa Nafasi ya TEKNOHAMA katika Kukuza Maudhui katika Tamthilia ya *Kigogo. Jarida la A / Mashariki la Masomo ya Kiswahili,* 5(1), 124-130.
Ngesa, A., Matundura, E., & Kobia, J. (2016). Mwingilianomatini katika tamthilia za Kiswahili: *Mashetani* na *Kijiba cha Moyo*. *Jarida la Kiswahili,* 22, 42-71.
Oruka, H. O. (2012). *Trends in Contemporary African Philosophy*. Nairobi Publishers.
Roman, A. (2019). Ujitokezaji wa Falsafa ya Ubuntu katika Riwaya ya Kiswahili: Uchunguzi wa *Adili na Nduguze* na *Siku za Watenzi Wote* (Tasinifu ya Umahiri). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
Samwel, M. (2015). *Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili: Mwongozo kwa Mwanafunzi na Mwalimu wa Fasihi Simulizi na Andishi*. Meveli Publishers.
Selemani, L. O. (2012). Riwaya Mpya ya Kiswahili na Masuluhisho ya Changamoto za Utandawazi (Tasinifu ya Umahiri). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
Senkoro, F. E. M. K. (2007). Uhalisiamazingaombwe katika Fasihi ya Kiswahili Istilahi Mpya Mtindo Mkongwe. *Jarida la Kiswahili la Isimu na Fasihi*, 21, 78-101.
Thomas, L. F. (2005). *The World is Flat*. Picador.
TUKI. (2019). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Oxford University Press East Africa Limited
Waters, M. (2001). *Globalization.* Routledge Taylor and Francis Group.